

Je,
**Mazingira
bora ya
kujifunzia**
yakoje?



Jishindie kompyuta
ndani!







Kweli? Basi shule yenu nzuri!
Natamani ningekuwa ninasomea
huko.



Kweli! Karibu.
Unaonaje
nikupeleke
Jumamosi?



Mh! Huwa mnaenda shule
hata Jumamosi?



Huwa kuna siku maalumu ya kusherehekeea mafanikio ya shule. Kila mtu anapaswa kwenda shule kusaidia kufanya usafi wa mazingira. Pia tunapanda miti siku hiyo.



Asante kwa mwaliko!



Shule nzuri kama ya Fatima ina mazingira masafi na mazuri na yenye kuvutia.



Mazingira masafi yanaweza kusaidia kukuza vipaji vya wanafunzi.



Je, mazingira mazuri na yenye mvuto ni yapi?





13

Mazingira mazuri yanajumuisha mambo mawili, mvuto wa kisaikolojia na mwonekano wake halisi.

1. Wanafunzi wana fursa ya kutoa maoni
2. Shule haina vurugu wala fujo
3. Kuna usawa wa kijinsia
4. Mazingira yake ni masafi na salama.

A pink ribbon banner is positioned at the bottom right of the page, attached to a wooden post. It contains the text "Hebu angalia mazingira yetu jinsi yalivyo safi na yenye mvuto!"

14



Na maoni yetu huchangia kuleta mabadiliko!

Kweli!! Sasa tuna maji ya kunawia mikono yetu!



Kuwa na sauti humaanisha kuwa tunashiriki katika kujirekebisha tabia wenyewe,



Tunashiriki katika kutunga sheria za darasani....

- SHERIA ZA DARASANI...**
1. Jali muda
 2. Kuheshimiana
 3. Uliza maswali
 4. Kuwa msafi
 5.

Tunashirikishwa katika
mipango mbalimbali ya shule



Kuwa na sauti pia humaanisha
kuwa tuna uhuru wa kujieleza!
Tunatoa maoni yetu.



Tunafanya mashindano ya
insha na midahalo,

Mashindano ya
Mdahalo

Mhuu! Huyo
ni noma!

...tunajifunza uigizaji



...tunajifunza muziki,

na michezo mbalimbali!



Kuwa na sauti humaanisha kuwa
maoni yetu yanathaminiwa.



Safi sana! Shule yetu pia ina
mazingira masafi na yenye
mvuto!



Hii ina maana kuwa shule yetu ina sera, sheria na taratibu zinazomlinda kila mmoja.



Inapotokea umeonewa, toa taarifa kwa mwalimu wa nidhamu au mwalimu mkuu.



Hatua zitachukuliwa kukusaidia na malalamiko yako yatakuwa siri.



Shuleni kwetu unyanyasaji wa kijinsia haukulbaliki!



Hakuna anayeruhusiwa kushika
sehemu zako za siri, kufanya au
kusema jambo litakalokufanya ujisikie
vibaya.

Njoo nyumbani
kwangu baada
ya masomo ...
nina zawadi
nzuri kwa ajili
yako!

Iwapo hali hiyo itatokea, toa
taarifa kwa mwalimu mkuu.



Watakulinda na kukomesha
tabia hiyo!



Kutokuwepo kwä ukatili humaanisha
kwä walimu wetu hawatutishi wala
kutufedhehesha wanapotuadhibu.

**Adhabu
ya viboko
haifai!**



Wanasisitiza adhabu isiyokuumiza



Safi sana!

Shule yetu pia ina
mazingira masafi na yenyemvuto!





Hii inamaanisha kuwa wasichana
hawapewi kazi nyingi zaidi kuliko
wawulana



Hawadhusumiwi wala kutukanwa



Hupewa mahitaji yao ya kibinafsi
pia

Samahani mwalimu,
ninaomba unisaidie
kitambaa cha kujisitiri


Haya, tumia
hizi!!

Na maji yale pale
kwa ajili ya kunawa






Tunahimiza ubora wa viwango vya juu




Kuna vyoo tofauti kwa ajili ya wasichana na wavulana




Na mazingira ni safi na salama!




Kuna viwanja vya michezo
mbalimbali



Kuna miti na maua mazuri!



Kuna vifaa muhimu vya
kujifunzia



Katika shule yetu,
tunachowaza...

Na tunavyohisi
ni muhimu sana
kwetu.



Shule nzuri inajali haki zetu ...





Je, utafanyaje ili kujenga mazingira mazuri na rafiki kwa mtoto?

- Weka sanduku la maoni
- Shirikisha wanafunzi katika kutunga sheria na taratibu za darasani
- Anzisha mashindano ya insha na midahalo
- Anzisha sera ya shule kuhusu ugomvi na unyanyasaji wa kijinsia
- Piga marufuku viboko
- Bandika kazi za wanafunzi darasani
- Vyoo na madarasa viwe safi muda wote
- Panda maua katika mazingira ya shule
- Anzisha siku maalumu ya kusherehekea ubora wa shule
- Tembelea shule nyingine na kujifunza
- Safisha mazingira ya shule kila wakati

Jinsi ya Kutumia Kitabu hiki

- Soma kitabu hiki kama sehemu ya mazoezi ya darasani
- Waulize wanafunzi na walimu kuorodhesha njia za kuawawesha wanafunzi kuwa na sauti
- Orodhesha mbinu za kuifanya shule kuepuka unyanyasaji na uonevu
- Orodhesha njia za kuwezesha mazingira ya shule kuwa masafi na salama
- Jaribu kutekeleza maoni yaliyopendekezwa
- Anzisha mashindano ya insha na midahalo kuhusu mada kama hii, "Mazingira ya shule huchangia kuboresha au kuathiri taaluma"
- Wahusishe walimu wengine kwa kufanya majadiliano katika vikao
- Jadili jinsi wavulana na wasichana wanavyolelewa shulenii. Je, wote wanapewa fursa sawa?

Toa maoni, shiriki na jishindie kompyuta!

Msomaji, Serikali yako inataku kukusikia! Shiriki kwa kutuma maoni yako. Mawazo yako yanaweza kuboresha huduma kwa jamii na utawala bora. Pia, hii itakuza ushirikiano kati ya wananchi na Serikali. Maoni yako yatahusiana na **mafunzo** uliyopata kupitia kitabu hiki. Kigezo cha kupata washindi ni ubunifu au wazo jipya.



Zawadi:



Kila baada ya miezi mitatu kwa mwaka 2012, maoni ya wanafunzi yatakayotumwa kupitia shule zao yatashindanishwa. Maoni kumi bora yatachaguliwa na yatachapishwa kwenye vitabu pamoja na tovuti. Kila shule itakayoshinda itapata kompyuta ndogo mbili (laptops).

Mwisho wa maoni yako weka taarifa zako:



- a) Tarehe
- b) Majina kamili, umri wako na jina la shule/taasisi
- c) Jinsia - Mwanaume/Mwanamke
- d) Anuani (SLP) kamili, makazi (Kata, Wilaya, na Mkoa)
- e) Simu yako na/au Barua pepe (kama unayo).



Unangoja nini! Shiriki basi kwa njia zifuatazo.
Tuma kwa:



- Barua: OGP Ikulu, S.L.P 9120 Dar es Salaam
- Barua pepe: ogp@ikulu.go.tz au opengovtz@gmail.com
- Tovuti: www.wananchi.go.tz

Fikiria. Paza Sauti. Twaweza!

MASHINDANO YA UIGIZAJI WIKI IJAYO! Usikose!



Mazingira
safi na
salama...

Kitabu hiki kimeandaliwa na:



Hujenga
ubunifu!

Jadili na wenzio ulichojifunza humu
au shiriki mjadala kuitia:



Twaweza_Nisisi



Twaweza Tanzania

www.twaweza.org

www.raisingvoices.org